

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam  
Tarehe 6 octoba 2007**

**Waliohudhuria**

Ally Saidi Mohamedi  
Aseli Wilison  
Elaine Baker  
Juma Ali Salehe Jongo  
Jumanne Idd Selemani  
Kibwana Mohammad Msiga  
Patrick Masinga  
Paulo Atibu Hatibu  
Sudi Saidi Ramadhan  
Yusufu Juma

**Mkutano na TANROADS**

Sudi Saidi, Elaine na Juma wamearifu kuhusu mkutano wa TANROADS tarehe 27 Septemba. Mahudhurio ya wana UWABA yalikuwa mazuri wanachama 12 walihudhuria. Tulipofika mkurugenzi wa maendeleo alituambia alipewa taarifa vibaya kwamba tulikuwa wengi mno, na hapakuwa na ukumbi wa mkutano na kwamba alikuwa na nusu saa tu kungea nasi. Pia alisema hapakuwa na kompyuta (laptop) wala projekta ambayo tungetumia Elaine hili na kusema kwamba hatukutendewa vyema kwani tumetumia muda mwingi kuandaa mkutano na kwamba tumepata barua ya mwaliko na bwana Isaack alituambia kwamba laptop na projekta zipo. Alisema kwamba hakutaarifiwa vizuri na bwana Isaack, alikubali kutusikiliza ingawa tulilazimika kufanya haraka kwani hakuwa na muda. Hii ilikuwa inachanganya na kuonyesha jinsi ambavyo TANROADS haiwajali wapanda baiskeli wala kusikiliza mawazo yao.

Meja aliwasilisha mada na kuwaita baadhi ya wajumbe walielezea hali ya barabara, na walifanya vizuri. Mwishoni mkurugenzi alisema kwamba masuala mengine hayakuwahusu TANROADS kama vile mwendo kasi au uegeshaji wa magari pembeni mwa barabara. Elaine alijibu kwamba TANROADS pia inahusika kwa sababu wangeweza kuweka viziwi ili kuzuia magari kuingia sehemu za waenda kwa miguu. Mkurugenzi wa Maendeleo hakuwa amepewa maelezo ya kutosha kuhusu barua tuliyoipata kutoka TANROADS na hakuweza kujibu maswali yetu badala yake alituambia tuyaweke kwenye barua nyingine.

Elaine aliandaa barua hii na wajumbe waliipitia na kufanya baadhi ya marekebisho. Dhumuni kuu ilikuwa kwamba ahadi waliyoipata TANROADS itekelezwe. Juma alisema angepeleka barua hiyo wiki ijayo.

Iliamuliwa kwamba tukutane na halmashauri ya jiji na askari wa usalama wa barabarani baada ya msafara baiskeli.

### **Msafara wa Baiskeli**

Elaine alisema kwamba clouds Fm walisema watatoa matangazo kwenye redio siku tatu kabla ya tarehe ya tukio lenyewe. Aliandaa maneno kwa ajili ya tangazo na wajumbe waliyapita na juma alisema atapeleka wiki ijayo clouds FM.

Elaine aliripoti kwamba ubalozi wa uholanzi wamesema watasaidia kwa kukodisha vyombo vya muziki, mahema na kununua zawadi ya bahati nasibu ya helimeti na majaketi atafuata fedha wiki hii.

Wiki hii tutafuatilia upatikanaji wa maji ya guta.

Juma alipeleka barua ya kuomba kutumia eneo la Mnazi mmoja bure tarehe 24 Septemba na atafuatilia majibu ya barua.

Tutanunua pia kupaza sauti (megafoni) ya nyongeza kwa ajili ya kutangaza wakati wa msafara.

Elaine alileta nakala za vipeperushi na mabango kwenye mkutano ambavyo shukuru alitoa nakala kwa kutumia fedha ya Elaine (atarudishiwa baadae na kupewa risiti)

Juma alishasambaza vipeperushi vingi.

Kila wanachama alichukua vipeperushi (kibwana 50, Sudi Saidi 50,Patrick 30, Juma 100, Ally Saidi Mohammed 20, Paulo 100 na Jumanne 20.) na mchango (Kibwana 20,Said Sudi 15, Juma 20, Ally Said Mohammed 10,Paulo 25, na Jumanne 10). Kila mwanachama atachangia gundi ya kubandika mabango hayo na watasambaza vipeperushi wiki hii na mabango na wiki ijayo watachukua vingine

### **Mchango kutoka Milan, Italia.**

La stazione delle biciclette ya Milan, Italia imetutumia barua pepe kwamba wanataka kututumia fedha walizokusanya kutoka a Bike Art Nouveau, Milan, Italia na kututumia picha za tukio Juma alikwenda benki kuchukua maelezo ya jinsi ya kuhamisha fedha na Elaine alituma barua pepe kwao.

### **Ofisi na Guta**

Elaine alishauri kusitisha kutengeneza ofisi hadi msafara utakapopita na tukiwa na muda wa kutosha.

Jumanne alimpa Juma Tsh 21,00 tarehe 22 septemba ambazo Juma alizitumia kutoa nakala za vipeperushi kwa tukio la michezo alilohudhuria. Jumanne hakuwa na malipo kwa wiki ijayo kwani ilitumika kununua tairi ya guta. Hili lilihojiwa kwani ilikuwa imewekwa wazi kwamba Tsh 500 kwa siku ilikuwa itumike kutengeneza guta Tsh 1,000 kwa siku iwe ya UWABA. Jumanne alisema atamwita dereva wa guta kwenye mkutano ujao ili aelezee.